Siku Kuu Ya Mama

. . . maskani, ndiyo maombi yangu. Hakika nina furaha asubuhi ya leo, kuona mteremko wa kiroho wa maskani hii, na jinsi hiyo, ishara huko nje, wanajitayarisha sasa kujenga kanisa jipya. Nafikiri linahitajika. Na angalia baada . . . kama Bwana Yesu akikawia, baada ya sisi kuondoka, watakuwa na . . . watoto wetu itabidi wapate mahali pa kwenda kanisani. Na tunataka "kuishindania kwa bidii Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Nafikiri hilo ni jambo jema.

2 Na nilipokuwa nikiingia tu, muda mfupi uliopita, kuongeza pamoja na shuhuda nyingi ambazo tayari zimetolewa kuhusu uponyaji, wa mikutano michache iliyopita, kwenye maskani hapa. Zinalundikana mara kwa mara, za uponyaji, uponyaji mkuu wa kimwujiza.

3 Nilikuwa nimemwacha mke wangu, sasa hivi, na watoto mla—mlangoni; na kulikuwa na dada, ameketi sasa, akiwa amesisimkwa sana mpaka akawa analia, mwujiza mkuu ulikuwa umetukia kwa mjukuu wake mdogo, huko chini kabisa, nadhani, kule Chattanooga. Bibi Nash, hapa, mjukuu wako mdogo alikuwa anateseka, na mkutano wa mwisho hapa, Bwana Yesu, nafikiri, alilitaja, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, ya kwamba, limekwisha. Na atakuwa mzima." Naye mvulana mdogo ni mzima kabisa na mwenye afya, vile tu awezavyo kuwa.

Na ina—inasisimua, unasikia shuhuda hizo.

4 Na kisha jamaa mmoja kijana, ambaye pia yupo, aliomba maombi kwa ajili ya Bibi Stotts, ambaye ndiyo kwanza amefanyiwa upasuaji. Na maslahi yao; unaona, kama hakuna mtu anayetaka tuwaombee, kwa nini wao . . . inaonyesha, mradi tu unajaribu, watu wakitaka uwaombee, basi wao, shauku, unaona. Wakati mwingine inakuwa mbaya sana, mpaka . . . sio mbaya, lakini nyingi sana, kwamba huna budi kukimbia tu mahali fulani na kuondoa kichwa chako, na kujificha kwa muda kidogo, ili kuishi. Lakini, ni—nina furaha wanafanya hivyo. Usifikirie kamwe kuwa sipendi kuwaona, kwa sababu kama wao . . . kama hakukuwa na mtu aliyetaka niwaombee, huduma yangu ingekuwa wapi? Unaona? Unaona?

5 Lakini wakati mwingine unaposema, "Ndugu Branham, sielewi watu wanapopiga simu namna hiyo, na—na unaponyokea mahali fulani." Yanipasa kufanya hivyo ili niweze kuishi, kuwaombea watu. Wewe huninii . . . Siyo—si mahali pamoja tu, hapa. Ni duniani kote. Unaona? Na—na ni mbaya sana. Na nina hakika kwamba unaelewa hilo.

6 Loo, ni vizuri sana kuwa Mkristo! Sijui ningefanya nini kama si Kristo, na hivyo . . . na kuwa na ushirika na Wakristo,

ambao, watu wenye Imani moja yenye thamani, wanaomwamini Mungu na wanamtumaini; na kuamini kwamba siku moja tukufu tutakuwa juu ya vita hivi vyote, na kupata ushindi, na kusimama tumekombolewa kwa mfano wake, upande ule mwingine.

7 Na kisha ningetaka kutoa tangazo fupi tu, ya kwamba, katika kuja kwa maskani, na kadhalika, mimi . . . tunafanya upya mfuko wetu, hasa sehemu yangu ya kampeni. Kote kwenye mikutano, tangu nilipoanza katika jambo hili, kwa upande wa kiinjilisti, miaka mingi iliyopita, badala ya kuanzisha mfuko, kuwa na kundi lingine la watu, nilitumia tu lile kundi nililolifahamu; na kutoka . . . na kuweka mfuko, ya kwamba mikutano yangu yote itafanywa chini ya jina la Maskani ya Branham. Na hiyo ingetumika katika Benki ya Kitaifa ya Muungano huko New Albany, kama mahali ambapo fedha zinaweza kulipwa—kulipwa kwa njia hiyo, kwamba haingetozwa kodi. Kama singefanya hivyo, pesa zote zilizochukuliwa zingetozwa kodi kwangu, kama singetumia Maskani ya Branham kama mfuko.

8 Wengi wenu mmenisikia nikitangaza hilo, mara kwa mara. Lazima niifanye, na . . . ili kufanya hivyo. Ndipo basi—basi tunaanzisha mfuko mpya sasa. Na tungependa wote wanaojua kwamba mimi . . . Ni wangapi waliowahi kunisikia nikitangaza jambo hilo, ya kwamba ibada zote, ninafanya kazi kupitia Maskani ya Branham? Inueni tu mikono yenu, nyote . . . Hakika, ninyi nyote. Ni nyote.

9 Na kwa hiyo ibada itakapokwisha, ukipenda, nina taarifa ndogo hapo, ili wewe, kama ungetia sahihi unapotoka. Ndugu Roy Roberson atakuwa nayo huko nyuma.

10 Maana, tutaweka mfuko mwingine, jambo lile lile, tu . . . lakini mfuko mwingine, ili fedha zetu zote na kadhalika, ambazo zimechukuliwa katika mkutano, zisitozwe kodi, itakuwa . . . inawekwa, kama kawaida, katika Benki ya Kitaifa ya Muungano, kuendeshwa kupitia maskanini, badala ya kuwa na ta—mfu- . . . mfuko mwingine. Maana, huu tayari ni mfuko, katika jina la Maskani ya Branham, mnaona. Na kwa hiyo kuna Branham *hapa* na Branham *pale,* na namna hii, na taasisi mbalimbali ambazo haziendi vizuri sana.

11 Ndugu Roberson atalishughulikia hilo, ninyi mtakaofanya, tunapotoka. Tutashukuru.

12 Sasa, asubuhi ya leo, kabla hatujaingia kwenye ibada, ningependa kusema, Bwana akipenda, kwamba nitajaribu kurudi tena usiku wa leo. Sipendi kuchukua mikutano yote miwili kutoka kwa Ndugu Neville, lakini ameniomba kwa ukarimu sana nizungumze tena usiku wa leo. Na kama Bwana akipenda, nataka kuzungumza usiku wa leo juu ya somo la uinjilisti, lenye mada hii: *Ni Nani Huyu?* Unaona? *Ni Nani Huyu?*

13 Na kwa hiyo asubuhi ya leo, nataka . . . Nilikuwa nikifikiria juu ya—juu ya kuzungumza asubuhi ya leo juu ya somo la Siku ya Mama. Nami ninajua kwamba alasiri ya leo na asubuhi zote zimejazwa na programu za Siku ya Mama. Kwa hivyo nilifikiri ningechanganya kitu, kwa sababu tunataka kuwaombea wagonjwa mara baada ya ibada hii kwisha, na kama kawaida.

14 Tunaamini ya kwamba Mungu ni mponyaji, na huwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Nami najua Yeye hufanya hivyo. Na ni zaidi ya ma—mashaka yoyote, hayo, maana kuna shuhuda nyingi sana zilizolundikana, ambazo tunajua jambo hilo.

15 Jana nilikuwa nikitazama kwenye gunia ambalo Ndugu Gene na Leo walikuwa tu wamehifadhi, la shuhuda walizookota. Nalo lilikuwa ni gunia kubwa lililojaa uponyaji wa ajabu, wa kimiujiza ambao Bwana amewafanyia watu.

16 Nami nikawaza, kama ingekuwa hivyo, vipi kama tungeweka hesabu ya yote yaliyotukia? Nadhani, huko Puerto Rico na Jamaica, peke yake, wangetoa elfu kumi, ama bora zaidi, shuhuda za ajabu, za uponyaji wa Bwana, alizofanya.

Sasa kabla hatujafungua Kitabu, hebu tuzungumze na Mwandishi.

17 Bwana, tunakushukuru sana, ya kwamba ni, tunapoinamisha vichwa vyetu, tunagugumiza tu maneno ya kusema; kwa maana siamini kwamba iko katika midomo ya mwanadamu kueleza hisia za moyo wa mwanamume au mwanamke, mvulana au msichana, ambaye amewahi kuwasiliana na Wewe. Kuelezea ibada zetu, jinsi tunavyokuabudu, na kile unachomaanisha kwetu. Imetutenga na dhambi, na ilitutenga na ulimwengu. Na inatupa kitu ambacho ni cha Milele na kilichobarikiwa. Na hatungeweza kupata maneno ya kutosha.

18 Kama ilivyosemwa wakati mmoja na mtu mheshimiwa, wiki chache zilizopita, kwamba angeweza kuzungumza kwa ufasaha katika takriban lugha tisa mbalimbali, akishikilia msimamo wake na mshauri wa Rais wetu mpendwa, Dwight Eisenhower. Na ingawa alikuwa na uwezo wa kuzungumza lugha tisa, kwa ufasaha; alisema, alipompokea Roho Mtakatifu, alijaribu kila tisa, na hapakuwa na maneno ambayo angeweza kupata, hakuna alichoweza kueleza, na hivyo Wewe ukampa lugha mpya ya kujieleza na kukushukuru kwayo. Nasi tunajisikia hivyo, pia, Bwana; kwamba, maisha yanapokwisha, kwamba labda tutazungumza kwa lugha tofauti, ili tuweze kueleza kile tunachofikiri kukuhusu Wewe.

19 Sasa tungeomba, Bwana, ya kwamba ungebariki maskani hii, mchungaji wake, wadhamini wake, mashemasi wake, washirika wake wote, watu wanaozuru hapa, wanaingia na kutoka milangoni. Na ionekane kila mara kuwa mahali pa

kimbilio palipowekwa wakfu, ambapo waliochoka wanaweza kuingia katika milango yake na kupata raha na amani kwa nafsi zao. Na ili wagonjwa waingie mlangoni, na kutoka wakiwa wazima, kwa sababu ya Uwepo udumuo milele wa Mungu Mwenyezi ambaye anakaa chini ya paa lake.

20 Tungeomba, Bwana, kwamba katika mpango huu ujao wa. . .hiyo inaundwa sasa, kwamba ungekutana na bodi na kukutana na wote. Na kama itakupendeza kwamba kuwe na ukumbusho wa daima wa maombi yaliyotolewa katika bwawa hili kuu, na lundo la magugu, siku moja; kwamba sasa imekuwa mnara wa taa, mahali pa kupumzika kwa waliochoka, kwa sababu ya jibu la maombi hayo.

21 Sasa utusamehe kwa jambo lolote tulilofanya, au kusema, au kuwaza, ambalo lilikuwa kinyume na mapenzi Yako makuu; pia kumbuka, Bwana, haikutoka mioyoni mwetu. Tunaweza tu kuwa tumeionyesha katika matendo yetu au kwa midomo yetu. Lakini, upesi, Wewe ulitusikia. Tulipoona tumekosea, tulikuwa tayari kuungama. Na hatutaki kushikilia katika mioyo yetu, uovu, basi tunajua kwamba Mungu hatajibu maombi yetu; lakini daima tuungame makosa yetu.

22 Nasi tungeomba, Bwana, ya kwamba ungebariki, asubuhi ya leo, kote nchini, inapoadhimisha siku hii ya ukumbusho wa Siku ya Mama. Lakini hii isiwe tu si—siku ya mama; kila siku iwe hivyo.

23 Mungu, jalia asubuhi ya leo kwamba akina mama, wanawake, ambao wamepotoka kutoka kwa Mungu, kwamba watajirudia wenyewe, asubuhi ya leo, na watatambua kuwa kile neno *mama* linachomaanisha, "aliyezaa." Na atambue kwamba wazao, kutokana na muungano wake na mumewe, wamekuwa vito vitakatifu ambavyo Mungu ameweka chini ya uangalizi wake. Kisha, Mungu atampa wajibu wa kulea watoto hao. Na kama Maandiko yasemavyo, ya kwamba, "Mwanamke mwema, na mama, kile alicho, kwamba watoto wake watamwita heri."

24 Ee Bwana, tunapoiona siku hii, wanapofika mbali sana na Maandiko, na kutenda karibu kama wanyama! Tunaomba, Mungu, ya kwamba utatupatia uamsho wa mtindo wa kale ambao utawaita warudi mahali wanapopaswa kuwa.

25 Bwana, hatungesahau, hata kidogo, kukushukuru kwa ajili ya mama halisi, kwa maana tunajua kwamba tunao kama hao wanaoishi leo hii; mama halisi, wa kweli. Mungu, awabariki. Wao ni hazina kuu kwetu, na tunaomba kwamba utaendelea kuwa pamoja nao, Bwana, basi jalia waishi kwa furaha na kuona matunda ya tumbo lao wakimtumikia Mungu.

26 Na tunaomba, Mungu, kwamba wale wanaovaa waridi jeupe asubuhi ya leo, ama ua jeupe, kusema kwamba mama yao amepita zaidi ya eneo hili la vitendo leo; naomba, Bwana Mungu,

wapumzike kwa amani na matendo yao yawafuate. Tujalie, Bwana.

27 Sasa chukua Neno Lako, Bwana, na useme na watu, na uwape faraja, kwa maana hiyo ndiyo sababu tumekusanyika hapa; kuhisi Uwepo Wako, kusikia Neno Lako, na kubarikiwa; na kutoka hapa tuwe wanaume na wanawake bora, wavulana na wasichana, kuliko tulivyokuwa tulipoingia. Tunaomba haya katika Jina la Yesu, Mwana wa Mungu. Amina.

28 Ninapenda usomaji wa Neno Lake lililobarikiwa. Kwa hiyo sasa tutafungua, asubuhi ya leo, katika Kitabu cha Wakorintho wa Kwanza, na kusoma kwa sehemu ya sura ya 15, kuanzia mstari wa kwanza.

> *Zaidi ya hayo, ndugu zangu, nawaarifu Injili niliyowahubiri, ambayo* nanyi *mmeipokea, na katika hiyo mnasimama;*
>
> *Ambayo kwa hiyo mnaokolewa, kama mkiyakumbuka* yale *niliyowahubiri, isipokuwa mmeamini bure.*
>
> *Kwa maana naliwatolea ninyi kwanza yale niliyoyapokea mimi, jinsi Kristo alivyokufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko;*
>
> *Na ya kwamba alizikwa, na ya kwamba alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko;*

29 Huenda ukasema, "Ndugu Branham, hilo ni somo lisilo la kawaida kwa ujumbe wa Siku ya Mama." Vema, hiyo ni kweli. Lakini, unajua, Mungu si wa kawaida, na Yeye hufanya mambo kwa njia isiyo ya kawaida.

30 Na nadhani, mawazo, ya mama. Nami ninaye asubuhi ya leo, kwa neema ya Mungu, angali hapa duniani pamoja nasi. Na ninashukuru kwa ajili ya mama. Lakini viumbe ambavyo tulipaswa kuwa navyo, pia, ibada ya uponyaji, na bila kujua ya kwamba ningerudi tena usiku wa leo, lakini nilifikiri labda tunaweza kuchora aina tofauti ya picha.

31 Mama ni mkuu sana. Unajua, wa kwanza kukupokea, katika maisha haya, ni mama yako. Hakuna mtu anayeweza kukugusa, kwa sababu umechukuliwa mimba, naye anakubeba chini ya moyo wake. Na yeye ndiye wa kwanza kukujua, na wa kwanza, katika maisha haya ku—kukushikilia. Kisha, unapozaliwa, yeye ni mmoja wa mikono ya kwanza ambayo inakugusa na kupangusa machozi kutoka machoni mwako. Yeye ndiye wa kwanza kukupigapiga na kukupenda, na kukubembeleza, katika maisha haya, ni mama yako. Sasa, nafikiri hakuna heshima ya kutosha ambayo tungeweza kumpa mama.

32 Mama ni wa kwanza na mtoto, na analo jukumu kubwa la kile mtoto huyo atakachokuwa, itategemea jinsi mama anavyomwanzisha mtoto huyo kwenye njia ambayo lazima aifuate. Mama analo jukumu, kutoka kwa Mungu, kumweka

mtoto huyo kwenye njia sahihi. Nami nafikiri ndiyo sababu akina mama wana mguso mdogo maalum.

33 Ninamjua mvulana katika jiji hili. Nadhani mama yake yupo sasa. Yeye ni karibu umri wangu. Lakini sisemi hivi ili kumuumiza mama yake; kwa sababu ana uchungu wa kutosha, kama akina mama wote. Lakini mvulana huyo hunywa pombe, na anakunywa sana. Na anapolewa sana, atakuja nyumbani na kuruka kitandani pamoja na mama yake na kumkumbatia. Naye ana wajukuu. Lakini kuna kitu kuhusu kikofi cha pongezi cha mama tu, ambacho kinaonekana kuchukua ma—mahali tofauti kuliko kitu kingine chochote kinachoweza kugusa; yaani, katika maisha haya, tukinena kibinadamu.

34 Unajua, mtu kama Musa, yeye. . . Ikiwa ningeweza kusifu chochote kwa tabia yake, ni kwa sababu alikuwa na mama aliyetumwa na Mungu. Unajua ni yeye aliyekuwa ameomba, Yokebedi, na kumtamani mtoto huyu. Na alipozaliwa, yeye ndiye aliyemtuliza, akamkumbatia na kujenga safina na kumweka katika nyasi, wakati maskini moyo wake ulipovunjika. Mtoto wake mdogo wa pekee, naye alikuwa ndiye ma—maskini kipenzi bora zaidi aliyekuwepo katika ulimwengu wote. Na jinsi mama anavyompenda mtoto yeyote! Lakini kumwona jamaa huyu maalum.

35 Na kisha, moyoni mwake, alijua kwamba alizaliwa kwa kusudi, na kisha kumchukua na kumweka kwenye pango lile lile la mamba, huko nje mtoni. Kwa imani alifanya hivyo, akijua ya kuwa Mungu aliweza kumtunza; na kujumlisha upendo wa mama, na tendo la tabia ya imani yake. Kwa maana imani haijiweki juu ya mchanga unaobadilika-badilika wa kile inachoweza kuona; imani inatulia kwa dhati juu ya mwamba usiotikisika wa Neno la Milele la Mungu. "Kwa maana kwa imani," Maandiko yanasema, "alifanya hivi."

36 Na imani inaweza kusimama juu ya mwamba, ya kwamba mawimbi yanaipiga misingi, na kutazama moja kwa moja kwenye uso wa kifo na kujua ya kwamba kitakuwa baada ya muda mfupi tu, lakini imani inaweza kumwangalia Yeye aliyesema, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima," na kukosa hata kusikia mawimbi yakiruka.

37 Hiyo ndiyo aina ya imani ambayo mama yake Musa alikuwa nayo. Alimfundisha na kumlea katika nyumba ya Farao, akimfundisha ya kuwa alizaliwa kwa kusudi, kwamba Yehova alikuwa amejibu maombi yake. Na, yeye. . . hangeweza kuwa na mwalimu bora zaidi. Hiyo ndiyo iliyosaidia kufinyanga tabia ambayo Musa alikuwa.

38 Ninaamini ni Abraham Lincoln ambaye aliwahi kutoa kauli kama hii. . .

39 Sasa, mimi si Mwanademokrasia au Mripablikan, mimi tu. . . mimi ni Mkristo. Kwa maana, nadhani upande mmoja

haungeweza kusema lolote dhidi ya upande mwingine; yote ni uozo. Lakini, Abraham Lincoln, kwa mawazo yangu, alikuwa mmoja wa...na alikuwa mmoja wa Marais wakuu ambao Marekani hii iliwahi kuwa nao; ikijumuisha Washington, na kadhalika.

40 Kwa maana, Abraham Lincoln alikuwa na mwa—mwanzo mbaya. Alikuwa maskini. Hakuwa na historia, kuhusu elimu, au—au kitu kikubwa, au pesa, au kitu ambacho kingeweza kumsaidia, kama Washington alivyokuwa nacho. Washington alikuwa mhitimu wa chuo kikuu, naye a—alijua; alikuwa mtu mwerevu, mtu mashuhuri, kwanza kabisa. Lakini Lincoln alilelewa katika kibanda kidogo cha magogo, chini ya maeneo mashuhuri ya Kentucky, na bila sakafu katika kibanda kidogo cha zamani, ambacho kiko kama ukumbusho hapa Louisville sasa. Lakini, akiwa mtu mashuhuri ambaye alikuwa, na ilimbidi ajifunze kuandika, juu ya ardhi aliyolima, ili kupanda mahindi.

41 Lakini ninaweza kuwapitishia hii vijana. Je, unajua Abraham Lincoln hakuwahi kumiliki kitabu maishani mwake, hadi alipokuwa na umri wa miaka ishirini na moja, ila Biblia na kitabu cha Foxe cha wafia imani? Unaona, unachosoma kinaumba tabia uliyo nayo. Si ajabu tuna kundi la wendawazimu leo; maskini magazeti ya zamani ya uongo, na uchafu na upuuzi, yamewekwa kwenye vibanda vyetu vya kuuzia magazeti. Alikuwa na Biblia na kitabu cha Foxe cha wafia imani. Angalia ni nini kilimfanya!

42 Lakini pamoja na hayo yote, siku moja alitoa kauli kama hii. Alisema, "Kama kunaweza kuwa na kitu chochote kizuri ndani yangu, ni kwa sababu ya mama mtauwa," aliyemlea kumtumikia Bwana.

43 Unaona, mtoto husikiliza mama yake; mguso mdogo kuhusu mama huyo, huo mtoto atasikiliza. Akiumia, ataenda kwa mama ili kufarijiwa kabla ya kwenda kwa baba. Kwa sababu, mama alikuwa naye kwanza, unajua. Na kuna karama fulani ambayo Mungu humpa mama, kuwa hivyo; ninamaanisha mama halisi. Sasa, ninaamini kwamba akina mama ni watu wa heshima na watauwa.

44 Lakini ninaamini, kama vile Sikukuu za Mama, namna hii, ni ulaghai, kutengeneza pesa nyingi kutokana na maua na kadhalika. Lakini siku ya mama inapaswa kuwa kila siku. Sio kumpelekea lundo la maua kwenye Sikukuu ya Mama, bali kumpenda na kumtunza siku mia tatu na sitini na tano usiku na mchana, mwaka mzima. Lakini, bila shaka, ulimwengu wa kibiashara una mshiko mkubwa katika mambo kama haya, nayo ina—ina—inapunguza thamani ya mama.

"Loo, vema, Sikukuu ya Mama iliyopita nilimtumia lundo la maua."

45 Angeshukuru, zaidi sana, kukaa tu chini na kuzungumza naye kidogo tu, mwandikie mstari, mpapase begani, mbusu shavuni, mwambie unampenda. Itaenda mbali zaidi kuliko maua yote ambayo unaweza kununua kutoka kwa muuza maua. Hiyo ni kweli.

46 Naamini ilikuwa katika Amri Kumi, marehemu Cecil DeMille, aliyeandika na kuweka kwenye skrini moja ya kazi bora zaidi za ulimwengu wa sinema. Na kabla haijawekwa jukwaani, au kutolewa nje, Cecil DeMille aliwaita Oral Roberts na Demos Shakarian, na kundi la wahudumu wa Full Gospel, na kuwapeleka kwenye studio zake mwenyewe na kuonyesha zile saa nne za Amri Kumi, na kuwauliza maoni yao juu yake. Mungu aipe raha nafsi yake shujaa!

47 Na nilipoiona, nilikuwa nikiitazama, na maelezo madogo daima yalinishika. Ikiwa wengi wenu waliona hayo, ilikuwa ni pale binti Farao...baada ya Musa kugundua kuwa yeye ni Mu—Mwebrania, na alikuwa ameamua kwenda kukaa na watu wake. Na hapo ameketi mama yake ambaye wakati mmoja alikuwa mrembo, amedhoofika, mwenye mvi na uso wake uliokunjamana, ameketi kwenye kiti cha zamani cha mikono; mama wa kawaida. Ndipo binti Farao akaingia. Naye akasema, "Mimi ni mwana wa nani, hata hivyo?"

48 Na ilipofunuliwa, kwamba Yokebedi alikuwa ndiye mama yake halisi. Binti Farao, na rangi yake na kadhalika, na kila kitu kikiwa kimepambwa; alisema, "Lakini, tazama! Anaweza kuwa mwanao, lakini," alisema, "Ninampa utajiri na fahari. Usingeweza kumpa chochote ila mashimo ya matope."

49 Lakini huyo mama mzee mwenye mvi akasema, "Lakini mimi nilimpa uhai." Hiyo huleta tofauti. "Nilimpa uhai." Mungu alimpa Uzima wa Milele. Kweli kabisa, mama!

50 Wakati mwingine watu huniambia, mara nyingi katika kampeni zangu, mimi "nahubiri daima juu ya ufufuo." Nami nilisoma somo asubuhi ya leo, mlango wa 15 na kifungu cha 4 cha Wakorintho wa Kwanza, juu ya ufufuo.

51 Lakini, unaona, jinsi wanavyomweka mama siku hizi, ni chungu cha maua kilichoketi karibu na bikizee, ambaye ni mzee na hawezi kuinuka, labda, na dhaifu, na mwenye mvi, na amejaa makunyanzi, na ameketi kwenye kiti cha mkono. Hiyo ni kweli vya kutosha. Lakini nataka kuchukua mada yangu na kukuchorea picha nyingine ya kile mama alicho.

52 Mtu fulani alisema, "Unahubiri kupita kiasi juu ya ufufuo. Karibu kila Ujumbe una jambo fulani kuhusu ufufuo."

53 Mbona, hakika. Ni—ni mahali pa muhimu pa Injili kupumzikia. Haijalishi alifanya nini, kama hakufufuka tena kutoka kwa wafu, basi yote yalikuwa ni bure. Hilo, kwangu, linathibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Mungu. Inathibitisha

kila dai alilotoa; ufufuo! Na pia ni mahali pa kutulia kwa nafsi. Ni mahali pa kuanzia. Ni kutiwa taji kwa faraja yetu.

54 Na tunapoona kwamba amefufuka kutoka kwa wafu, inatuweka sisi, tukiwa na silaha za Injili, kwenye uwanja wa vita, kuchukua mahali, kupiga vita. Kwa maana, tunajua Yeye alisema, "Yule atakayeipoteza nafsi yake kwa ajili Yangu ataipata tena."

55 Nami nafikiri ni kutawazwa kukuu kwa Injili Kamili, ni ufufuo, na ahadi zake za Kiungu, na faraja inayowapa wale wanaoitumainia. Kwa maana, inaahidi muungano mkuu wa kuungana kwetu pamoja tena. Inaahidi, na ku—kufifia kwa dhambi zote. Inaahidi kufifia kwa ulemavu wote, mateso yote ambayo tumekuwa nayo katika hili, iliyobidi tupite nayo, katika maisha haya. Inaahidi, na kutoweka kwa yote. Inaahidi kwamba hata kifo kitapoteza uwezo wake, nasi tutafufuka katika mfano wa Yesu. Kwa hiyo, kwa maoni yangu, ufufuo ndiyo ahadi kuu kuliko zote katika mambo ya Maandiko. Hapo ndipo ilipoyatia muhuri.

56 Na Pasaka iliyopita, nilipokuwa nikihubiri juu ya mambo matano ya:

> Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
> Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
> Lakini, alipofufuka, alihesabia haki bure
> milele.

57 Hiyo ndiyo Siku kwa ajili yangu, ile Siku kuu ya siku! Na kuona kile itakachomaanisha, kwetu sote, katika ufufuo, tunapofanya kazi na kuingojea ile Siku iliyobarikiwa ya siku!

58 Inatupa ahadi kwamba siku moja hawa akina mama wazee, wanyonge, dhaifu, wenye mvi, waliovurugika watabadilishwa. Sio tu kwamba mama atakaa pale, peke yake, lakini familia yake yote pamoja naye.

59 Na itakuwa siku iliyoje! Itakuwa ni wakati ulioje, tutakapotazama nyuso za wale ambao tumewapenda sana! Ni tofauti ya namna gani asubuhi hiyo, tutakapowaona wapendwa wetu, na—na kutazama watakavyokuwa wakati huo! Mateso yote yataondolewa. Mateso yote yataisha. Hakuna tena mashavu yanayoonekana dhaifu ya kifo. Hakuna machozi zaidi kutoka kwa macho. Ufufuo unaahidi yote haya. Hakutakuwa na matanga tena. Hakuna tena kumpigapiga mtoto kwenye shavu, hiyo ni kama kipande cha jiwe; ambapo mtayarisha mazishi ameupaka dawa, na kusukumwa nje na kupaka rangi, na kadhalika, kuonekana kawaida. Haitahitajika tena, huko.

60 Ndipo ninawazia juu ya tunapowaona wamesimama kule, wapendwa wetu, mama zetu, jamaa zetu, marafiki zetu wote; na kuwaona katika miili yao isiyoweza kufa, miili yao ya mbinguni; kuangalia tabia zao, kuona jinsi wanavyojiendesha kwa utamu na utulivu huo, hakuna woga au kufadhaika tena.

Kuwaona wakati huo wakisimama katika sura ya Bwana Yesu, hiyo itakuwa ni siku ya ajabu.

61 Na kila mmoja wetu, katika akili zetu, anatazamia na kutamani saa ile ya faraja, tutakapokutana nao. Kila mmoja anawazia mpendwa wake, labda mama yao ambaye ameenda. Na itakuwa ni siku iliyoje, utakapomwona tena! Na kwa baba, na kwa kaka, na kwa . . . wapendwa wote, itakuwa siku iliyoje!

62 Ninawazia, pia, sasa hivi. Ninawazia familia yangu, itakuwa na maana gani kwangu Siku hiyo.

63 Ninafikiri kwamba, katika asubuhi hiyo ya ufufuo, labda wa kwanza atakuja kukutana nami atakuwa mtoto wangu Sharon. Hapana, hatakuwa anatetemeka. Ibilisi huyo hawezi kuingia mahali hapo. Hakuna homa ya uti wa mgongo inayoweza kugusa Nchi hiyo. Hatakuwa ananipungia mkono kwaheri. Macho hayo madogo ya samawati, yatakuwa yakicheza huku akitupa mikono yake mbele na kupiga mayowe, "Baba!" Nitafurahi kumwona, kujua kwamba hatakufa tena; kujua ya kwamba yote yamekwisha, ndiyo sababu ninahubiri ufufuo kwa nguvu sana.

64 Kisha nitamwona mama yake, mama yake Billy, mvulana wangu. Na nina kumbukumbu nyingi huko ambazo zinaendelea. Nakumbuka nilipokuwa nikimchukua; ama Bw. Combs, hapa juu, alikuwa akimchukua kwa safari ya mwisho, nami nilikuwa nikimfuata, kwenye gari. Tulipokuwa tukishuka kwenye Barabara ya Saba, pale pale; Billy, umri wa miezi kumi na minane.

65 Jinsi wangemleta nje mtaani, na kumruhusu amwone. Naye alikuwa akilala na kulia, na kumwangalia mtoto wake mchanga, lakini hangeweza kumkaribia.

66 Na kisha njiani kuelekea huko, mtayarisha mazishi akaja na kushuka kwenye—kwenye—kwenye Mtaa wa Saba. Mama hapa alikuwa akimtunza wakati huo. Naye alikuwa amesimama nje uani, na maskini suruali fupi, na kofia ndogo nyekundu iliyovutwa upande juu ya kichwa chake. Na wakati mama huyo, akiwa amelala kwenye kitanda kile, nyuma ya gari hilo la kuchukulia wagonjwa, akinitazama, alipomwona mtoto wake mchanga amesimama uani, akijua alikuwa akifanya safari yake ya mwisho; aliinuka kutoka kwenye kitanda na kupiga mayowe, na kutupa mkono wake wenye mifupa, kumkumbatia mtoto wake mchanga uani. Lakini hakuweza kuwa naye.

67 Loo, itakuwa furaha kumuona siku hiyo. La, hatakuwa na mikono yenye mifupa, wala hayo mashavu hayatabonyea ndani. Lakini atasimama katika uzuri wa mbinguni wa malkia wa Mbinguni, na wa mama. Macho yake meusi, meusi kama mbawa za kunguru, yatakuwa yanacheza kwa furaha. Hatainama kabisa; ambapo, huyo shetani wa TB hataingia kwenye hiyo Nchi. Lakini, asiyeweza kufa, atasimama katika mfano Wake.

68 Nadhani, basi, mwingine atakayekuja kukutana nami atakuwa Edward, ambaye tulimwita "Humpy," kwa jina fupi. Alikuwa ndiye wa kwanza wa mnyororo mkubwa wa viungo tisa, mnyororo wa familia ya Branham. Alikuwa kiungo cha kwanza kuvunjika; aliye karibu nami. Nitamwona Edward akinijia mbio. Walakini, alikufa akiwa mvulana, mwenye umri wa miaka kumi na tisa. Na ninapomshika mkono, nina hakika tutakuwa na mambo mengi ya kuzungumza juu yake, ya ujana, maana tulikuwa marafiki. Tulishikamana pamoja. Aliniruhusu nivae suti yake, na—na—na mambo, kama ndugu halisi walivyofanya. Itakuwa furaha kumwona tena.

69 Na nitamsikia akisema kitu kama hiki, "Ulipata neno langu, Bill? Ulikuwa ukifanya kazi kwenye shamba la mifugo, wakati wa kuondoka kwangu duniani. Lakini hospitalini, nilituma ujumbe, 'Mwambie Bill kila kitu kiko sawa.'"

Nitafurahi kusema, "Ndiyo, nilipata ujumbe wako, huko nje kwenye mbuga."

70 Kisha, nadhani, anayefuata atakuja baba yangu. Alikuwa ndiye kiungo kinachofuata cha kwenda, na . . . Hapana.

71 Nadhani Charles alikuwa ndiye kiungo aliyefuata, kaka mdogo. Alipata ajali ya gari akiwa mvulana mdogo tu. Kila mara aliweka dawa mguu wake wa kulia alipokuwa akitembea. Lakini, unajua, ninapomwona, hatakuwa akiburuta mguu huo. Yote yataondolewa, atasimama katika fahari ya kijana.

72 Naye ataniambia, kitu kama hiki, anapotabasamu. Atasema, "Ndiyo, Bill, hakuna ajali huku juu. Na ninakumbuka usiku kabla sijachukuliwa kwenye ajali ya gari, ulizungumza nami, tumesimama kwenye barabara ndogo ya nyumba yetu ndogo," na ninatazama juu, hivi sasa. "Ulizungumza nami kuhusu Bwana, saa chache tu kabla ya kwenda. Nawe ulikuwa mimbarani ukihubiri nilipoondoka."

73 Kisha atakuja baba. Loo, naweza kumwona. Ingawa alinichapa viboko vingi vikali, kile hasa nilichohitaji, lakini nitaona mshtuko huo wa nywele nyeusi za mawimbi, nzuri zaidi kuliko hapo awali, siku hiyo. Naye atanitazama, na kusema, "Mvulana wangu, unajua, Baba hatasimama kutoka kwenye meza hapa tena, akiwa na njaa, kuwaacha watoto wake wale, maana hapa tunacho kwa wingi. Kamwe hakuna upungufu hapa."

74 Kumwona wakati angefanya kazi, na kwa senti hamsini au sabini na tano kwa siku, na kisha kuinuka kutoka mezani ili watoto waweze kula, kurudi kazini tena. Naye alifanya kazi kwa bidii sana mpaka shati lake lingeuchoma mgongo wake kwa jua, na mama angelikata kwa mkasi.

75 Nitamsikia akisema kitu kama hiki, "Bill, unakumbuka usiku ule wewe na Ndugu George mlikuja kuniombea nilipokuwa ninaenda? Unajua, nilimwambia mama kwamba

kulikuwa na Malaika wawili weupe wamesimama kwenye kitanda, na malaika mwekundu miguuni. Na yule malaika mwekundu alikuwa akijaribu kunichukua, lakini Malaika mweupe alisimama katikati. Hatimaye walinipeleka Nyumbani."

76 Halafu, pia, anayefuata kwenye kiungo cha kwenda, au aliyeenda, atakuja Howard. Nitamwona Howard; tulipokuwa tukitembea pamoja kote nchini, kila mahali; aliyeitwa kuwa mhudumu; mtu mwaminifu, lakini washirika wake walimzuia. Mazungumzo ya mwisho niliyofanya naye, alisema, "Nikienda, Bill . . . "

77 Ni—nilimwona akienda, kwa ono, yapata miaka minne kabla hajaenda. Nikamwambia nilimwona Pop akiweka alama kwenye kaburi lake na kusema hilo ndilo lililofuata.

78 Naye akasema, "Kuna jambo moja nataka unifanyie." Alisema, "Nimeyachanganya maisha yangu. Nimeoa na kila kitu. Si—sijui nini kimetokea."

Nikasema, "Je, unamwamini, Howard?"

79 Akasema, "Kwa yote yaliyo ndani yangu, ninamwamini." Katika yapata siku mbili ama tatu kabla hajaondoka, alifanya amani yake na Mungu, pamoja na Ndugu Neville na hao wengine pale. Naye akasema, "Kuna jambo moja nataka ufanye. Nikienda, Bill, waambie waniimbie, *'Ataelewa, Na Kusema, "Umefanya Vizuri."'"*

80 Ninaamini, kabla sijampa mkono Howard, nitamsikia akisimama na kunitazama, na kusema, "Bill, alielewa."

81 Baada ya hayo, atakuja Ndugu Seward, Ndugu Frank Broy, Ndugu George DeArk. Loo, ufufuo unamaanisha mengi kwangu. Natarajia saa hiyo kuu ya kutiwa taji. Na Nuru inapoanza kuenea, "Tutajua kama tunavyojulikana." Tutaelewa, na—na tutawakumbuka rafiki zetu na wale—wale ambao wamekuwepo.

82 Na—na wengi, kutakuwa na wengi huko ambao hatukufikiria hata kuwa huko. Kwa maana, unajua, ni wakati huo, ambapo naamini kwamba "mkate tuliotupa juu ya wanadamu, maji ya taabu, yatatarudia Siku hiyo." Tunapoona athari za ushuhuda wetu, juu ya watu ambao hatukuelewa hatua yao kuelekea Kwake, labda watakuwepo. Hiyo itakuwa Siku iliyoje!

83 Na halafu, pia, zile mbegu tulizopanda, bila hata kufikiria kile wangefanya, lakini hizi hapa. Zilitoa matunda ya thamani, na tutaziona Siku hiyo, wapenzi wapotovu na jamaa.

84 Na ninafikiria juu ya maelfu ambao nimewaona wakiongoka, naam, kuwa mamilioni sasa, wakienda, na kilichokuwa huduma yao. Loo, itahitaji zaidi ya ufufuo. Itahitaji Umilele, kuzunguka huku na huko, kupeana mikono na kutafuta mambo ambayo sijui sasa.

85 Kutakuwa na wale akina mama wazee wenye mvi, ambao mmevaa hayo maua meupe kwa ajili yao leo, kwamba watawaona, na watakuwa wa kupendeza. Sio kuwakilishwa na chungu cha maua, au picha fulani ya mtu mzee mwenye kichwa chenye mvi; lakini katika sura na uzuri wa ufufuo, watasimama kwa mfano wa Kristo, miili yao ya mbinguni, vijana na wa kupendeza milele. Hakika, hayo ndiyo mengine. Hiyo ndiyo Siku ya akina mama ninayongojea. Huko ndiko kutawazwa. Sio karafu kwenye pazia, lakini kutawazwa kwa roho, kwa maana Mungu amembadilisha!

86 Ninamwazia mama yangu mwenyewe, mkongwe na dhaifu, huku anatetemeka kwa kupooza. Hatafanya hivyo Siku hiyo. Itakuwa tofauti basi. Na hiyo Nuru kuu inaanza kuenea, tunapoanza kutazama huku na huku, na duara kubwa litakuwa linazidi kuwa kubwa zaidi na zaidi. Yote ni kuonyesha tu mbinu ya Yesu. "Na baada ya muda," kama wimbo ulivyosema, "nami nitamwona Yesu hatimaye."

> Atakuwa akiningojea, Yesu, mwema sana na wa kweli.
> Juu ya Kiti Chake kizuri cha Enzi atanikaribisha Nyumbani
> Baada ya siku hii kuisha.

87 Kisha tunapomwona, nasi hatutakuwa kama tulivyo sasa. Tuta—tutajua jinsi ya kumpenda Yeye zaidi. Hatutasimama nyuma kwa hofu kidogo; kwa sababu, tutakuwa kama Yeye. Vema, Yeye atakuwa wa jamaa yetu zaidi kuliko alivyo sasa. Tutamuelewa vizuri zaidi. Kwa sababu, tuko mbali sana, katika miili ipatikanayo na mauti; basi tutakuwa na mwili kama mwili Wake mtukufu. Tutajua jinsi ya kumwabudu. Na tunapoona yale Uwepo wa Utu Wake umetufanyia, ulitubadilisha; wazee wanarudi kuwa vijana, wote waliopindika wananyooka. Loo! Tutaelewa basi kwa nini nguvu Zake zilituponya.

88 Maswali ambayo yamekuwa akilini mwetu, "Anawezaje kufanya jambo hilo? Itafanya nini *hii?*" Kwa njia fulani, kiajabu, zote zitatoweka. Vifundo ambavyo vimefungwa nyuma ya akili zetu, "Je, itakuwa hivi? Inaweza kuwaje?" Kwa njia fulani, au nyingine, vidole vikubwa vitatenganisha tu, kufunua mafundo hayo, na yote yatafifia katika taji moja kubwa la upendo.

89 Kisha tutamwona. Kisha tutakuwa kama Yeye. Kisha tutamuabudu Yeye. Ndipo tutamwona mama jinsi Mungu anavyomtaka.

Mama asingekamilika Huko bila familia yake.

90 Maana, wakati mkuu zaidi wa maisha yake yote ni kuwaona watoto wamezunguka meza, na wote wenye afya na furaha; na—na—na kumwona akimimina kahawa, ama chochote anachofanya, na kutengeneza chakula cha jioni, na yeye na baba

waketi. Mbona, huo ndio wakati wa furaha zaidi maishani mwa mama, kuwaona watoto wake wote nyumbani.

91 Sasa, usikose, usikose Siku hiyo. Acha mnyororo mkubwa wa familia yako uunganishwe pamoja, kiungo kwa kiungo. Hebu kila njukuti iwe kwenye gurudumu. Kisha tunapoketi pamoja na jamaa zetu na makundi yetu, kuvuka dari za Umilele, hiyo itakuwa Siku ya jinsi gani! Ndipo tutaelewa.

92 Ilikuwa ni Yeye aliyeahidi jambo hili, katika Ufunuo 1, ambapo ilisema, kwamba, "Upanga mkali wenye makali kuwili ulitoka kinywani Mwake." "Aliitwa Neno la Mungu." Na ilitoka kwenye midomo ile ile, ambayo ilisema, "Mimi Ndimi niliye hai, niliyekuwa nimekufa; na mimi ni hai milele." Kutoka kwenye midomo iyo hiyo, katika Yohana Mtakatifu 6, thelathini-. . . inasema hivi, kwamba, "Sitapoteza chochote, bali nitakifufua tena katika siku za mwisho." Ilikuwa ni Yeye aliyetoa ahadi; midomo hiyo hiyo ya thamani. Yeye Ndiye Yule atuokoaye, atuponyaye, aliyetukomboa, na atakayetufufua siku ya mwisho.

93 Ikiwa wewe ndiye kiungo dhaifu ambaye ametenganisha muungano huu mkuu wa familia katika Siku hiyo, naomba Mungu wa Mbinguni, asubuhi ya leo, kwa namna fulani kwa njia ya ajabu, afunue hayo mafundo madogo ambayo yamefungwa akilini mwako, na akufunulie upendo alio nao kwako, na uje kwa utamu kumtumikia Yeye.

Tunapotafakari juu ya mambo haya, tuombe.

94 Kabla tu hatujaomba, nanyi mmeinamisha vichwa vyenu, nitawaulizeni. Je, mngependa, kwenye hii Siku kuu ya Mama, kuyaweka wakfu upya maisha yenu Kwake, mkitarajia ufufuo huo? Je, mwaweza kumwinulia mikono yenu? Wakati kila mtu . . . Mungu akubariki.

95 Je, kunaweza kuwa na mwenye dhambi ambaye yuko sasa, angesema, "Ee Mungu, bado sijajiunganisha kwenye kiungo hicho. Mimi ndiye niliyepotea ambaye hangekuwapo wakati mama anaenda kutazama huku na huko kote Utukufuni. Sitakuwepo, kwa maana bado sijapata amani na Mungu. Sina tumaini la Uzima wa Milele ndani yangu. Lakini leo ni— ninataka kufanya hivyo"? Hivi waweza kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham, wakati huu. Ninataka kukumbukwa katika maombi, kwa maana nina wapendwa ng'ambo ya bahari, bahari ya Uzima, na ninataka kukutana nao"? Inueni mikono yenu.

96 Au mtu fulani ambaye amerudi nyuma, na angetaka kurudi siku hii, na kusema, "Bwana, najiweka wakfu tena Kwako; nikija kufanya upya agano langu na Wewe," mwaweza kuinua mikono yenu?

97 Baba yetu wa Mbinguni, inapokaribia, siku hii itafanya siku moja karibu zaidi na tukio hilo kuu. Na tumelazimika, kila mwaka, kuona hili likiwakilishwa.

98 Kama vile watu walivyokuwa wakipanda kwenda Yerusalemu Siku ya Pentekoste, na kwa ajili ya kutakasa maskani na mahali patakatifu, na—na sadaka ya dhambi; kila mwaka walikumbushwa, wakati yule mwana-kondoo alipokufa huko nje, kwamba ungekuja wakati ambapo Mwana-Kondoo wa Mungu angekufa, kuachana na dhambi. Kila wakati maskini jamaa huyo alipolipuka, na damu ikanyunyiziwa mikononi mwao, walikumbushwa kwamba kungekuwa na wakati ambapo kutakuwa na Mwana-Kondoo wa Mungu, ambaye angelia, "Eli, lama . . .? Eli, lama . . .?" msalabani.

Ninaomba, Mungu, kwamba tunapotazama leo na kuona jambo hilo . . .

99 Wiki chache zilizopita, kabla ya kuondoka katika huduma Yako, kuelekea California, Indiana hii ilikaa tupu na imekufa, na hapakuwa na uhai, ilivyoonekana. Maua ambayo yalikufa msimu uliopita wa kupukutika. Majani yalikuwa yametoka kwenye miti. Na utomvu kwenye miti ulikuwa umeingia kwenye mizizi, na kila kitu kilikuwa kimekufa.

100 Lakini kulikuwa na msimu ambapo jua lilianza kuangaza kwa njia tofauti. Jua lile lile lililokuwa limeangaza wakati wa baridi kali, lakini vipengele vilibadilika na kuangaza tofauti. Na kwa kung'aa kwa jua, pamoja na vitu vya asili, uhai ulichipuka, kila mahali. Majani yakarudi kwenye miti. Tawi . . . Uhai uliokuwa umetoka kwenye jani, na jani likadondoka, bali uhai ukaingia ardhini; lilirudi katika uzuri mpya, katika uzuri wa ujana. Ua ambalo lilikuwa limetoa ha—harufu yake nzuri, ambalo lilikuwa limetoa uzuri wake wa kung'aa na kuanguka chini; lilizaliwa, likatokea tena katika ujana wake, na harufu mpya.

Je, tunakumbushwa nini, Bwana, saa hizi?

101 Na dunia ikatoka kwenye jangwa tupu, lenye giza, ikawa paradiso ya uzuri, na nyuki na ndege wakiimba, na kila kitu kuwa na furaha, na miti i—ikivuma kwa upepo wa upepo wenye joto wa masika. Joto na furaha vilikuwa duniani tena, kwa sababu ya jua, j-u-a.

102 Lakini siku moja yule M-w-a-n-a yuaja na uponyaji katika mbawa Zake, na hayo maisha madogo ambayo yamefichwa kama utomvu kwenye mti, ardhini, kama u—uhai ulio katika mbegu ya ua, utaifanya kuwa mpya tena, isififie kamwe. Loo, jinsi tunavyokushukuru kwa hili!

103 Na kulikuwa na mikono mingi, mingi sana iliyoinuliwa asubuhi ya leo, maana wanajua kuwa ng'ambo ya pazia huko, kuna kitu. Wanatamani kumwona mama. Wanatamani kuona wapendwa wao na marafiki zao, na kujua siri hizi zote, jinsi walivyokuja hapa, na kote katika wakati. Yote iko nyuma ya pazia lililofichwa. Na siku moja Wewe utakuja. Na wakainua mikono yao; wao—wao—wao—wanataka kuwa na

hakika, Bwana. Wanajifanya upya tena, vivyo hivyo na mimi. Sasa tusaidie, Bwana. Ifanye upya imani yetu na nguvu zetu.

104 Na tunapohisi ujio wa Bwana. Na miaka arobaini iliyopita, pentekoste mpya ilizuka duniani. Roho akaanza kufunua mambo. Na hapa tuko kwenye ile ishara ya mwisho, kabla tu ya kule Kuja. Tunajua ujio wa Bwana umekaribia. Na tunawaona wagonjwa wakiponywa kutokana na maradhi yao, ambayo imekuwa ya ajabu kwa ulimwengu, kwa miaka elfu mbili, tangu mitume. Lakini hii hapa inatokea tena, manabii wakitokea, Malaika wanatokea, ishara na maajabu. Ni nini? Ufufuo unakaribia. M-w-a-n-a anakuja.

105 Jalia tuwe tayari, Bwana. Hebu tukumbatie kila ahadi ya Kiungu; usifikirie kuhusu haya mafundo madogo ambayo yamekusanywa na sayansi, na kadhalika, kwamba haiwezi kutukia. Hebu waanze kufumuka, asubuhi ya leo, kwa kutokufa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . anapotetemeka katika Maneno ya Biblia ya Mungu, kama chombo kilichopangwa vizuri, ili kuimba wimbo, "Mimi ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai hata milele." "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; lakini ninyi mtaniona Mimi." "Kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." "Na itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, ya kwamba nitamimina Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; ishara na maajabu; wazee wataota ndoto, na vijana wataona maono," ishara ya mvua ya vuli na wakati wa mwisho. Jalia ihisiwe miongoni mwetu, asubuhi ya leo, Bwana, pia jalia imani yetu ihifadhiwe. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Siku Kuu Ya Mama SWA59-0510M
(Mother's Day)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza kwenye Siku kuu ya Mama, mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 10 Mei, 1959, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org